Kiambatanisho Cha III: Barua ya Human Rights Watch Kwa Waziri wa Katiba na Sheria Waziri Augustine Mahiga, Disemba 24, 2019

Mheshimiwa Augustine Mahiga, Waziri
Wizara ya Katiba na Sheria
Mji wa Serikali, Mtumba
S.L.P 315 Dodoma
TANZANIA

Kwa Fax: +255 26 2321679
Kwa Barua Pepe: km@sheria.go.tz

Disemba 24, 2019

Mpendwa Mh. Waziri Augustine Mahiga:

Tunakuandikia kwa niaba ya Human Rights Watch, shirika la kimataifa linalonukuu ukiukwaji wa haki za binaadamu katika nchi zaidi ya 100 ulimwenguni kote na kufanya kazi na serikali katika kuboresha usimamiaji wao wa haki za binadamu. Hivi karibuni, Human Rights Watch imenakili taarifa juu ya haki ya afya nchini Tanzania, hasa ikiangazia namna gani sheria na sera zimezuia makundi maalum, hasa wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wengine na watu wenye jinsia tofauti na asili, kunufaika na haki yao ya msingi ya kupata huduma bora ya afya iliyopo, kama inavyohakikishwa na sheria ya kimataifa. Hii ndio mada ya ripoti inayotarajiwa kutoka, na tungependa kuipatia ofisi yako fursa ya kupitia na kujibu matokeo ya utafiti wetu wa awali kufikia tarehe 10 Januari 2020, ili kwamba tujumuishe mtazamo wa serikali katika ripoti yetu itakayochapishwa.

Ripoti ni matokeo ya mahojiano na wanawake wanaofanya mapenzi na wanawake, wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume, wanaovutiwa mapenzi na jinsia zote mbili na watu wenye jinsia tofauti na asili(LGBT) wapatao 35 ambao wamekuwa wakiathirika moja kw amoja na sheria na sera ambazo ripoti inazichambua, pamoja na mashirika mengine ya Kitanzania, kikanda na kimataifa na wataalamu na wahisani wa masuala ya afya na haki za

binaadamu na mashirika ya Umoja wa Kimataifa. Wakati ripoti imejikita katika haki ya afya, ripoti itajadili pia ukiukwaji wa haki zingine unaowakabili wana-LGBT nchini Tanzania, ikiwa ni pamoja na ukamataji holela, vipimo vya lazima vya njia ya haja kubwa, na ukiukwaji wa haki ya uhuru wa kutengenza vyama/mashirika. Kama unavyofahamu, siku za hivi karibuni tulichapisha ripotu juu ya vitisho kwa vyombo vya habari na asasi za kiraia nchini Tanzania, ambayo ilijumuisha baadhi ya mijadala ya ukiukwaji wa haki za uhuru wa kushirikiana/kutengeneza mashirika kama jinsi inavyoathiri makundi yanayofanyia kazi afya na haki za LGBT.[311]

Tunaambatanisha pia baadhi ya matokeo ya utafiti wetu, yakifuatiwa na maswali ili yatuwezeshe kuelewa msimamo wa serikali. Tunawasiliana na Wizara ya Afya moja kwa moja, ukizingatia kwamba ukiukwaji mwingi wa haki za binadamy unatokana na sera za wizara. Hata hivyo, kwasababu ya wajibu wako wa kulinda haki za binadamu za Watanzania wote, tungependa pia kukueleza wasiwasi wetu kuhusiana na sera ya afya ambayo haiendani na haki za msingi .

Upatikanaji wa Huduma za Afya Maalum, Zisizo za Kibaguzi

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ya Tanzania Baraimevifunga vituo vya msaada ambavyo vilikuwa vinatoa huduma maalumu za VVU kwa makundi maalum ikiwa ni pamoja na wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wenzao na watu wasio na jinsia ya asili, na imezuia mashirika ya kijamii kufanya warsha juu ya VVU kwa makundi haya. Wengi wa wana-LGBT tuliowahoji wamesema matokeo yake, hawana tena huduma za afya za kirafiki, zisizokuwa za kibaguzi. Wameripoti matukio mbalimbali ya ubaguzi wa chuki dhidi ya LGBT walipokuwa wakitaka kupata huduma za afya katika vituo vya afya/hospitali za serikali.

Kwa mfano, Mwanaume anayevutiwa kimapenzi na mwanaume mwingine mwenye umri na miaka 24 na muathirika wa VVU alituambia kwamba muhudumu wa afya katika Hospitali ya Sinza Palestina, ambapo alikuwa anapata matibabu ya VVU, alimwambia: “Wewe ni kijana mzuri, kwanini unafanya mapenzi na wanaume wenzako? Ndio maana umepata UKIMWI, kwasababu hayo matendo yanamchukiza Mungu.” Muhojiwa huyo aliongeza “Waliniambia pia kwamba niache hii michezo na kuokoka, nimfukuze Shetani,

[311] Human Rights Watch, *“As Long as I am Quiet, I am Safe”: Threats to Independent Media and Civil Society in Tanzania*, Oktoba 28, 2019, https://www.hrw.org/report/2019/10/28/long-i-am-quiet-i-am-safe/threats-independent-media-and-civil-society-tanzania.

anayenisababisha kufanya maoenzi na wanaume, na kupata mke, nioe na kuwa na familia." Hatimaye aliipata NGO inayotoa huduma za afya rafiki kwa wana-LGBT, lakini kwa muda aliepuka kabisa kupata huduma za afya: "Sikutaka kuisogelea kabisa hspitali ile kwasababu ya ukatili wao."[312]

Mwanaume mwingine anayevutiwa kimapenzi na mwanaume alituambia alipoenda Hospitali ya Mwananyamala Septemba 2018 kupima VVU, wahudumu wa afya pale "hawakufurahia nilipowaambia kwamba mimi ni mwanaume ninayevutiwa kimapenzi na mwanaume mwingine…. Walikuwa wanatumia lugha mbaya – 'kama wewe ni mwanaume unayevutiwa kimapenzi na mwanaume mwingine, wakati mwingine usije tena katika hospitali hii, kwasababu hatutibu watu kama wewe.'"[313]

Tutashukuru kupata majibu yako kwa maswali yafuatayo:

Nini wajibu wa Wizara ya Katiba na Sheria katika kuhakikisha haki ya usawa kwa Watanzania wote, kama vile ilivyoahidiwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mikataba ya Kimataifa ya haki za binadamu ambayo Tanzania ametia sahihi?

Ni hatua gani ambazo Wizara ya Katiba na Sheria imezichukua kuhakikisha kwamba wana-LGBT hawakumbani na unyanyapaa na ubaguzi wanapokwenda kupata huduma za afya katika vitui vya afya/hospitali za serikali?

Kuna utaratibu wowote ambao wana-LGBT wanawaweza kuripoti kwa usalama na bila kujulikana vitendo hivyo vya unyanyapaa na ubaguzi katika sekta ya afya ikiwa watakutana navyo?

Upimaji wa Nguvu wa Njia ya Haja Kubwa

Human Rights Watch iiliwahoji wanaume watatu nchini Tanzania ambao walifanyiwa vipimo vya nguvu vya njia ya haja kubwa. Kwa mujibu wa mjumbe maalum wa Umoja wa Mataifa anayeshughulikia mateso, "Katika nchi ambazo mapenzi ya jinsia moja ni kosa la jinai, wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wenzao wako hatarini kufanyiwa vipimo

[312] Mahojiano kati ya Human Rights Watch na Osman (jina bandia), eneo limehifadhiwa, Mei 22, 2018.
[313] Mahojiano kwa njia ya simu kati ya Human Rights Watch na Suleiman (jina bandia), Oktoba 2, 2018.

vya lazima vya sehemu ya njia kubwa vinavyolenga kupata Ushahidi wa kimwili wa mapenzi ya jinsia moja, kitendo ambacho hakina maana kitabibu na ni sawa na mateso."[314] Human Rights Watch imewahi kuripoti huko nyumba jinsi gani vipimo vya njia ya haja kubwa havina thamani yoyote ya kitabibu au kisayansi na husababisha msongo wa mawazo wa muda mrefu kwa wale wanaokumbana na udhalilishaji huu.[315]

Tungependa kupata majibu yako kwa maswali yafuatayo:

Nini msimamo wa Wizara ya Katiba na Sheria katika matumizi ya vipimo vya nguvu vya njia ya haja kubwa kama Ushahidi wa vitendo vya ngono vya kukubaliana? Je wizara inaviafiki au kuviruhusu vipimo vya njia ya haja kubwa katika mazingira yoyote yale ambayo vipimo vinafanyika bila ya ridhaa ya mtu anayepimwa?

Je Tanzania itazuia vipimo hivi vya nguvu vya njia ya haja kubwa kwa madhumuni ya kushitaka suala la mapenzi ya jinsia moja, katika mazingira yoyote yale?

Uvamizi wa Holela katika Mikutano na Warsha

Tangu mwaka 2016, polisi wamevamia mikutano na warsha zilizoandaliwa na wanaharakati wa afya na haki za binadamu, huku wakiwakamata washiriki eti kwa tuhuma za "kuhamasisha ushoga." Hakuna kosa kama hilo chini ya sheria za Tanzania, na polisi hawajawahi kufanikiwa katika mashtaka dhidi ya washiriki katika kesi nyingi za hivi, lakini uvamizi huu una madhara mabaya kwa asasi za kiraia, zikituma ujumbe kwamba hata mikutano ya kujadili kujikinga na VVU miongoni mwa wana-LGBT ni kinyume na sheria. Matukio haya ni pamoja na:

- Disemba 14, 2016 polisi walivamia mkutano uliokuwa Protea hotel jijini Dar es Salaam, wakiwakamata washiriki nane na kuwahoji ikiwa mkutano ulikuwa "mkutano wa wanaume wanaovutiwa kimapanzi na wanaume." Wanasheria

[314] Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, "Report of the Special Rapporteur on torture and other cruel, inhuman or degrading treatment or punishment," A/HRC/31/57, Januari 5, 2016, http://www.refworld.org/docid/56c435714.html (imepitiwa Mei 19, 2016), aya. 36.

[315] Human Rights Watch, *Dignity Debased: Forced Anal Examinations in Homosexuality Prosecutions*, Julai 12, 2016, https://www.hrw.org/report/2016/07/12/dignity-debased/forced-anal-examinations-homosexuality-prosecutions#5f63ba.

walifanikiwa kuwatoa siku hiyo hiyo, lakini polisi ilishikilia vitambulisho vyao kwa siku kadhaa.[316]

- Septemba 15, 2017, polisi Zanzibar walivamia warsha iliyokuwa imeandaliwa na shirika moja la kijamii kwa wazazi wa watu kutoka makundi maalum juu ya kujikinga na kujitibu na VVU, ikiwakamata washiriki 20, watu wanaojitolea, na wafanya kazi, kwa misingi ya "kuhamasisha mapenzi ya jinsia moja." Kumi na nane kati yao waliachiwa pasipo mashtaka siku hiyo hiyo, wakati wawili walibaki wameshikiliwa kwa siku mbili.[317]
- Oktoba 17, 2017, walivamia warsha ya maswala ya kisheria iliyokuwa ikifanyika Peacock Hotel jijini Dar es Salaam, na kuwakamata watu 13, ikiwa ni pamoja na wanasheria wa Afrika Kusini na Uganda na wanaharakati waliokuwa wakiliwakilisha shirika la Initiative for Strategic Litigation in Africa (ISLA), wawakilishi wa shirika la afya na haki la CHESA, na wanaharakati wengine wa Kitanzania. Walishutumiwa kwa "kuhamasisha mapenzi ya jinsia moja" na kushikiliwa kwa wiki nzima.[318]

Tutashukuru tukipata majibu yako kwa maswali yafuatayo:

Ni kwa misingi gani ya sheria polisi walivamia warsha na mikutano hii kuhusu maswala ya haki za afya na za binadamu na kuwakamata washiriki?

Je Wizara ya Sheria iko tayari kuchukua hatua kuhakikisha kwamba uvamizi na ukamatwaji huu unakomeshwa, ikiwa ni pamoja na kufafanua hadharani kwamba kufanya mikutano juu ya afya na haki ya makundi maalum si kosa chini ya sheria ya Tanzania?

---

[316] Mawasiliano ya barua pepe ya Human Rights Watch, Disemba 14 na Disemba 18, 2016; Andrew Green, "In an Apparent Crackdown, Tanzania Government Raids NGO Meeting on Reproductive Rights," *Devex*, Januari 6, 2017, https://www.devex.com/news/in-an-apparent-crackdown-tanzania-government-raids-ngo-meeting-on-reproductive-rights-89394 (imepitiwa Septemba 22, 2019).

[317] Mawasiliano ya barua pepe kati ya Human Rights Watch na mtetezi wa haki za binadamu Zanzibar, Oktoba 24, 2019; University of Pretoria Center for Human Rights na Pan Africa ILGA, "Press statement: Centre for Human Rights and Pan Africa ILGA express grave concern about threats to the right to freedom of association and right to information as twenty are arrested at training workshop in Zanzibar, Tanzania for alleged homosexuality," Septemba 20, 2017, https://www.chr.up.ac.za/news-archive/1225-press-statement-centre-for-human-rights-and-pan-africa-ilga-express-grave-concern-about-threats-to-the-right-to-freedom-of-association-and-right-to-information-as-twenty-are-arrested-at-training-workshop-in-zanzibar-tanzania-for-alleged-homosexuality (imepitwa Julai 18, 2019).

[318] Wendy Isaack, "Facing Prosecution for Challenging HIV Policies in Tanzania," andiko la Human Rights Watch, Oktoba 20, 2017, https://www.hrw.org/news/2017/10/20/facing-prosecution-challenging-hiv-policies-tanzania.

Tutashukuru majibu yako juu ya maswali haya na taarifa zingine za ziada juu ya msimamo wa serikali kuhusiana na mwenendo wa haki ya afya, haki ya kushirikiana (kutengeneza shirika), haki ya kutokuteswa na kufanyiwa unyama, vitendo vya kinyama na kushusha hadhi kwa wana-LGBT kufikia Januari 13, 2020. Inawezekana tukashindwa kujumuisha majibu yenu yatakayo pokelewa baada ya tarehe hiyo katika ripoti yetu inayotarajiwa kutoka hapo baadae. Tafadhali tuma majibu hayo kwa mtafiti mwandamizi, Neela Ghoshal, kupitia [redacted]

Tunasubiria kwa hamu mahojiano mazuri katika kupigania haki ya upatikanaji wa huduma bora zaidi za afya kwa Watanzania wote, bila kujali mwelekeo wao wa kingono au utambulisho wa kijinsia.

Wako Mwaminifu,

Graeme Reid
Mkurugenzi, Programu ya Haki za LGBT

Mausi Segun
Mkurugenzi Mtendaji, Idara ya Afrika
Human Rights Watch